


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA



Unapojuji tafadhali taja:
Kumb. NA. AB. 156/423/01

Tarehe: 24 Mei, 2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI KWA MKATABA **(MUDA WA MWAKA MMOJA)**

Mkurugenzi wa Jiji la Arusha anawatangazia Watanzania wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Jiji la Arusha kutuma maombi ya kazi ya muda wa mwaka mmoja kwa Mkurugenzi wa Jiji ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili. Nafasi hizi ni za mkataba wa muda wa mwaka mmoja.

1. Dereva II (Nafasi 13)

Sifa Zinazotakiwa

Awe na Elimu ya kidato cha nne na Leseni ya daraja E au C1 ya uendeshaji wa magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali. awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari (basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya ufundi stadi(VETA)au chuo kingine kinachotambuliwa na serikali.

Kazi na Majukumu ya Dereva

- a) Kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali na usalama wa gari.
- b) Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari.
- c) Kufanya usafi wa gari.
- d) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- e) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.

Malipo:

Mshahara kuwa katika ngazi ya mishahara ya Serikali yaani **TGS B**

2. Mgambo wa Jiji (Nafasi 15)

Sifa Zinazotakiwa

Awe na elimu ya kidato cha nne, na cheti cha mafunzo ya Mgambo. Awe raia wa tanzania wenyе umri kati ya miaka 18 na 25 mwenye afya njema kiakili na kimwili mwenye macho ya kumbukumbu za kupatikana na hatia ya makosa ya jinai,uwezo wa kusoma na kuandika kiswahili na kingereza.

Kazi na Majukumu ya Mgambo wa Jiji

- a) Kulinda na kudumisha usalama wa Halmashauri na mali zake.
- b) Kulinda watu na mali zao katika eneo la Halmashauri.
- c) Kusimamia utekelezaji wa sheria Kanuni na taratibu zilizopo.
- d) Kufanya doria maeneo mbalimbali ya Halmashauri.
- e) Kutuliza fujo inapotokea tukio linaloashiria uvunjifu wa amani katika eneo la halmashauri.
- f) Kushiriki kazi za misako katika Halmashauri.
- g) Kushiriki katika matukio ya dharura piandi yanapo jitokeza.
- h) Kulinda misafara ya viongozi wanapotembea maeneo ya Halmashauri.

Mshahara:

Mshahara utakuwa ngazi ya mishahara ya Serikali yaani **TGOS A**

MAELEZO YA JUMLA.

- a) Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania wahitimu wa vyuo mbalimbali.
- b) Waombaji wawe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45
- c) Barua za maombi ziambatanishwe na nakala za maelezo binafsi (CV) vyeti vya Elimu/taaluma na cheti cha kuzaliwa.
- d) Nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA).
- e) Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Jumatatu ya tarehe **05/06/2023 saa 9:30 alasiri.**

Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi,
Halmashauri ya Jiji la Arusha,
S.L.P. 3013,
ARUSHA.

Tangazo hili limetolewa na:

Hargeney R. Chitukuro
MKURUGENZI WA JIJI
ARUSHA

Nakala; - Kwenye mbao za Matangazo

